OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA OR – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

Barua zote ziandikwe kwa Mkuu wa Shule

Email: info@kikaro.sc.tz

✓ **Email: emmyjkn@gmail.com**

Website: www.kikaro.sc.tz

SIMU:0789021005/0784587853

Kumb: Na. KSS/Admn/vol-07/2022.

Mkuu wa Shule,

Shule ya Sekondari Kikaro

S. L. P 48, CHALINZE

10/May/2022

JINA MWANAFUNZI ……

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023

Kichwa cha habari hapo juu cha husika:

Uongozi wa shule ya sekondari kikaro inafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya sekondari kikaro karibu.

Nafurahi kukufahamisha kuwa ,umepangiwa mchepuo wa **CBG/ HGL/ HGK/HKL** (Kata isiyostamili). Natumia nafasi hii kukupongeza kupata nafasi hii adhimu ambayo wengi wanaitamani na wameikosa. Bila shaka hutaipoteza "HONGERA SANA". Unatakiwa kufika shuleni ***TAREHE……. (ITAKAYOTANGAZWA NA WIZARA).***

Shule ya Sekondari Kikaro ipo mkoa wa **Pwani,** Halmashauri ya Chalinze katika kata ya Miono. Ukitoka Dar es salaam, panda magari yaendayo ***Saadani au Miono*** katika kituo cha daladala cha ***MBEZI YA KIMARA*** nauli ni Tsh 9000/=. Ukitokea barabara ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga unatakiwa kushuka kituo cha **Mandera Kibaoni** kabla ya kuvuka mto wami**.** Hapo utapanda gari nyingine kwa nauli Tsh 2000/= au pikipiki kwa tsh 5000/= tu, na utafikishwa hadi shuleni. Ukitokea barabara ya Morogoro (hasa kwa wanaotokea mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Shinyanga n.k) utashukia kituo cha CHALINZE kisha utakwenda stand ya Tanga na utapanda gari nyingine zinazoelekea MIONO kwa nauli ya shilingi 5000/= tu.

Hakikisha unakuja na nakala ya RESULT SLIP na nakala ya cheti chako cha kuzaliwa.

Pamoja na barua hii, naambatanisha fomu za maa gizo maalum; fomu hizi ni;

1. Fomu ya kukubali nafasi ya kidato cha Tano Shule ya Sekondari Kikaro
2. Fomu ya kupima Afya yako (iwe na muhuri wa Mganga Mkuu wa Mkoa/ Wilaya au Kituo cha Afya)
3. 3. Fomu ya mahitaji ya shule

KUMBUKA : Fomu namba (1) na (2) ukikamilisha kuzijaza uje nazo shule siku ya kuripoti.

Mkuu wa shule na wafanyakazi wengine wote wa shule hii wanakutarajia uwe mwanafunzi mtiifu, mwaminifu, nadhifu na mshiriki wa kazi zote za nje na ndani ya darasa.

ANGALIZO Hakikisha unafika shuleni ndani ya wiki ya kwanza ya kufungua shule na. sivinginevyo

……..

EMMANUEL JOHN KAHABI.

MKUU WA SHULE.

FOMU NA. 01

HALMASHAURI YA CHALINZE

ANWANI YA MZAZI/MLEZI ,

S . L .P …….

EMAIL ……

TAREHE ……/……/20 …..

MKUU WA SHULE,

S.L.P 48

CHALINZE.

YAH: **UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2021/2022 SHULE YA SEKONDARI KIKARO.**

SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI)

Mimi (jina kamili) …… (Tahasusi ……..……) niliyezali wa tarehe …… Mwezi…… Mwaka …… Dini ……katika Kijiji cha …… Wilaya ya …….. Mkoa wa……

Nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha tano ***Shule ya Sekondari Kikaro***. Pia nitatii sheria na miongozo yote ya shule ambayo mwanafunzi anatakiwa kutekeleza hususani kufaulu vizuri na kutomiliki simu shuleni.

SAHIHI YA MWANAFUNZI ……TAREHE …….

SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI)

Mimi …….. (Jina kamili) w a Kijiji/Mtaa …….. kata ya ……..Wilaya ya ……Mkoa wa ……Dini……
Kazi yangu ni ……

Nafurahi sana kupokea nafasi aliyopewa mwanangu. Nitatekeleza na kutimiza maagizo yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya shule. Pia nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na shule katika kumlea mtoto huyu kitaaluma, kinidhamu na kimaadili na hata miliki simu akiwa shuleni na ikitokea amekamatwa na simu afukuzwe shule kwa mujibu wa sheria.

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI …… TAREHE ……..

SEHEMU C: (IJAZWE NA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI/MTAA/ KATA)

JINA…….. SAHIHI …….
TAREHE…….. MUHURI……

FOMU NA: 2

HALMASHAURI YA CHALINZE

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KIKARO

S.L.P. 48.

…. /…. /202…

MGANGA ……

HOSPITAL/KITUO CHA AFYA ……

S L . P ……

YAH: <u>KUPIMA AFYA (MEDICAL EXAMINATION)</u>

Tafadhali mpime ……

Kama afya yake inamruhusu kuendelea na masomo ya Sekondari kidato cha Tano mwaka 2021

Andika NDIYO au HAPANA katika nafasi zilizoachwa wazi mbele ya ugonjwa kama aliugua.

1. Kifua Kikuu ……
2. Ugonjwa wa moyo ……..
3. Ugonjwa wa figo ……..
4. Ugonjwa wa akili ……..
5. Ajali kubwa ……
6. Pumu ……..
7. Vidonda vya tumbo ……..
8. Kifafa ……
9. Kupasuliwa ……..
10. Mengineyo

……

……

……

<u>MAELEZO YA MGANGA</u>

……

……

JINA LA HOSPITALI /KITUO CHA AFYA ……

JINA MGANGA…… SAHIHI ……

TEREHE …….. MUHURI ……

SARE YA SHULE

i. Suruali za dark blue 02, **ZIWE NA MARINDA MAWILI**, zisiwe models upana wa chini usipungue 18'' (wavulana) huvaliwa darasani

ii. Suruali nyeusi 02, zisiwe models upana wa chini usipungue 18'' (wavulana) huvaliwa muda wa nje

iii. Mashati meupe mikono mirefu mawili (02) kwa wavulana na wasichana

iv. Viatu vya ngozi vyenye gidamu jozi mbili (02) rangi nyeusi (Wavulana na wasichana)

v. Wavulana huvaa tai rangi ya dark blue na wasichana huvaa skaff

vi. Sketi mbili ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu, mshono wa V mbele rangi ya dark blue (wasichana)

vii. Sketi mbili ndefu rangi nyeusi zenye malinda ya kawaida kwa ajili ya kushindia (wasichana) viii. Viatu vya ngozi jozi mbili (02) rangi nyeusi ix. T – Shirt (02) zenye nembo ambazo huvaliwa darasani kila siku ya jumatano.

x. T – Shirt (02) za kushindia na zenye nembo ya shule ambazo huvaliwa baada ya muda wa darasani.

xi. Truck suti full rangi ya dark blue yenye jina la shule (zinapatikana mazingira ya shule) xii. Shuka mbili (cotton) za blue bahari kwa wavulana na rangi pink kwa wasichana

xiii. Sweta rangi ya dark blue hasa kwa wale wenye matatizo ya kifua/upumuaji.

xiv. Kila mwanafunzi ni lazima aje na nguo za michezo, wavulana waje na jezi nyeusi ya Taifa stars pea moja na wasichana waje na jezi nyeupe ya taifa stars pea moja.

xv. Kila mwanafunzi ni lazima aje na viatu vya michezo (wavulana raba nyeusi na wasichana raba nyeupe)

VIFAA VINGINE

i. Sanduku la bati na kufuli lake kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.

ii. Godoro moja futi mbili na nusu kwa sita lenye ujazo wa inchi 4 (2½ x 6 x 4'') yanaweza patikana mazingira yanayoizunguka shule.

iii. Kila wanafunzi ni lazima aje na chandarua (nyeupe kwa wasichana na blue kwa wavulana) iv. Sahani, kijiko bakuli, kikombe na ndoo (02) za lita kumi kwa ajili ya matumizi binafsi na dumu moja la kuhifadhia maji ya kunywa la lita 20

iv. **Kila mwanafunzi ni LAZIMA aje na RIMU mbili nyeupe za karatasi A4 pindi anaporipoti shuleni**

v. Vifaaa vifuatavyo kila mwanafunzi avilete kutokana na tahasusi yake:

CBG	Hard broom	Toilet brush	Fyekeo (kwanja)
HGL	Soft broom	Squeezer	Fyekeo (Kwanja)
HGK	Ufagio wa cherewa za mti	Squeezer	Fyekeo (kwanja)
HKL	Hard broom	Soft broom	Jembe

NB: Ili kuepuka usumbufu katika usafiri wa umma, kuna baadhi ya vifaa vinapatikana karibu na maeneo ya shule na bei zake zinafanana na maeneo mengine, unaweza kuwasiliana na idara ya mapokezi kujua ni vifaa vipi ili uepukane na usumbufu huo.

MICHANGO YA SHULE

JINA LA AKAUNTI: KIKARO SECONDARY SCHOOL. AKAUNTI NA: NMB 21101100021

NO.	AINA YA MICHANGO	KIASI	MUDA WA MALIPO
01	ADA YA SHULE WAWEZA LIPA KWA MUHULA	70,000.00	KWA MWAKA
02	KUCHANGIA TAALUMA	20,000.00	KWA MWAKA
03	MTIHANI WA MOCK	20,000.00	MARA MOJA TU
04	UKARABATI	15,000.00	KWA MWAKA
05	MATIBABU	10,000.00	KWA MWAKA
06	KULIPA WAPISHI NA WALINZI	30,000.00	KWA MWAKA
07	TAHADHARI	5,000.00	KWA MIAKA MIWILI
08	KITAMBULISHO NA PICHA	6,000.00	MARA MOJA TU
09	NEMBO YA SHULE	2,000.00	MARA MOJA TU
JUMLA		**178,000.00**	

❖Michango yote ni lazima ilipwe Benki ya NMB. kiasi cha shilingi **108,000/=kilipwe** muhula wa kwanza na kumalizia **70,000.00** muhula wa pili.

JINA LA AKAUNTI: KIKARO SECONDARY SCHOOL. AKAUNTI NA: NMB 21101100021 **TAWA LA BENKI: NMB CHALINZE**

❖ **Malipo yote yafanyike kupitia akaunti ya shule na sio vinginevyo.**

MAWASILIANO

- ❖ **Mkuu wa shule**: 0789021005
- ❖ **Makamu Mkuu wa Shule**: 0788 776 331 au 078458785
- ❖ **Mapokezi (Admission)** 0764718417au 0789400229 au 0686718584:

Kwa maelekezo zaidi tafadhali tembelea Tovuti ya shule : www.kikaro.sc.tz

MAWASILIANO YA MZAZI NA MWANAFUNZI YATAFANYIKA KUPITIA NAMBA HIZI.

- ❖ **MATRON** 0683502546, 0744738112 na 0656945312 kwa Wasichana tu.
- ❖ **PATRON** 0785070840 ,0688978779, 0785480658 kwa wavulana tu.

KWA UFAULU MZURI KWA MTOTO WETU, UONGOZI WA SHULE UNASHURI MZAZI/MLEZI KUMNUNULIA VITABU VIFUATAVYO ILI VIWEZE KUMSAIDIA

ORODHA YA VITABU AMBAVYO MZAZI ANASHAURIWA KUMNUNULIA MWANAFUNZI

Orodha ya vitabu vifuatavyo hutumika kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari kwa kidato cha tano na sita. Kila mwanafunzi anatakiwa kununua baadhi ya vitabu hivyo kwa kila somo kwa masomo aliyopangiwa

ENGLISH LANGUAGE -I

- Asheri, N. (2014) Advanced Level English: A Practical Approach 3rd Edition., Dar es Salaam: Good Books Publishers
- English Language for Secondary School, Language &usage – form five&/six (TIE)
- Advanced English Language: form five &six by Oxford.
- Advanced English Oxford/Longman Dictionary

ENGLISH LANGUAGE II

- English Language for secondary school, Literature &stylistics- Form five and six (TIE)
- Ashel , N (2011), Advanced level literature. The Essential guide: Good Book Publishers, DSM
- Advanced Level Literature (2008) Nyambari Nyangwine Publishers, DSM

POETRY

- Selected Poems. - Tanzania Institute of Education
- ***NOVELS AND SHORT STORIES*** The Wonderful Surgeon and Other Poems. (Aje na vitabu viwili kati ya hivyo– Charles Mloka)- Mkuki na Nyota Publishers Ltd
- The Beautyful Ones Are Not Yet Born - Ayi Kwei Armah
- A Man of the People - Chinua Achebe
- Divine Providence - Severin N. Ndunguru
- His Excellence Head of State - Danny Safo
- Encounters from Africa – Macmillan Education Limited

PLAYS (Aje na vitabu viwili kati ya hivyo)

- Betrayal in the City - Francis Imbunga
- I Will Marry When I Want - Ngugi wa Thiong'o and Ngugi wa Mirii
- Lwanda Magere - Okoiti Omtatah
- An Enemy of the People - Henrik Ibsen (e) Black Mamba - John Ruganda

HISTORY

- TIE (2016*) History for Secondary Schools: Form Five* - Tanzania Institute of Education.
- *Understanding Africa in the New World History. History Paper II Notes*. By Antony E Tungilayo 'Mzilikazi'
- *Contemporay Historical Events, Advanced Level History II*. By Comred Shibitali C.K Tumaini
- Tumain$_{\text{Sons publishers}}$i, S.C.K (2010) *Contemporary Historical Events: Advanced Level History one*, Dar es Salaam: Shibitali &
- Yassin Salehe *(..) Essentials in Advanced Levels History Paper 2*, Dar es Salaam

KISWAHILI

- *Nadharia ya lugha ya Kiswahili1: Kidato cha Tano na Sita* – Nyambari Nyangwine na Masebo (2010)
- Saluhaya, M.C. (2016*) Nadharia ya Lugha Kidato cha Tano, Sita na Elimu ya Juu,* STC-Publishers.Dar es Salaam.
- James john na Mduda F (2014*) Kiswahili Kidato cha Tano na Sita,* Oxford University Press.
- *Kamusi Kuu ya Kiswahili* - BAKITA
- *Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita* – Masebo – Oxford university Press
- *Tahakiki Vitabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6* – Nyambari Nyangwine na Masebo

TAMTHILIA (Uje na vitabu viwili kati ya hivyo)

- Kivuli Kinaishi – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press
- Kwenye Ukingo wa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
- Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)
- Morani –Emanuel Mbogo (1993)

RIWAYA (Uje na vitabu viwili kati ya hivyo)

- Vuta N'Kuvute, 4th ed. – Sharif Adam Shafi
- Kufikirika, 4th ed. – Shaban Robert – Mkuki na Nyota
- Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
- Usiku Utakapokwisha, 2nd ed. – Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

USHAIRI) (Uje na vitabu viwili kati ya hivyo)

- Kimbunga: Toleo la Tatu (3rd ed.) – Haji Gora Haji (1995) – TUKI
- Mapenzi Bora – Shaban Robert – Mkuki na Nyota publishers
- Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan

GENERAL STUDIES. (Uje na kitabu kimoja kati ya hivi)

- Secondary School Education Joannes BigirwaMungu &Sospeter M. D eogratias. *Understanding Advanced Level General studies*; Advanced
- Nyangwine, C.M, Bukagile G.R & Maluka S.O (2010) *Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies Notes form 5 & 6*

GEOGRAPHY

- *Geography for Secondary Schools: Form Five.* - Tanzania Institute of Education (2016)
- *Intergreted Aproach (Physical Geography)*
- *Practical Geography: Map-reading, Photograph, Research and Surveying*. – Zisti Kamili
- *Elementary Physical Geography: Advanced Level and Colleges*. – Ahmed Lubwama
- Msabila, DT (2000) *An Integrated Focal Regional Study on Human and Economic Geography.*
- *A Comprehensive Approach to Physical Geography* – D.T. Msabila

BIOLOGY

- Gleen and Susan Toole (1999) *New Understanding Biology for Advanced Level 4th edition.*Nelson Thornes. United Kingdom

  Taylor D.J etal (2017*) Biological Science 1&2 3RD Edition*. Cambridge University Press
- Susan Toole & G. Tool e*. Understanding Biology for A - level students*
- B.M. V Roberts. Biology*: A functional Approach*

CHEMISTRY

- Inorganic part I & II by TIE
- Physical chemistry - Mzumbe book project
- Chemistry by Chande.
- Physical chemistry - Ramsden

- A - level Calculations - Ramsdens
- Chemistry by Petrus
- Organic Chemistry part (A & B) (Mzumbe BK project).
- Organic Chemistry by Solomon.
- TIE (2019) General Chemistry for Advanced Level Secondary Schools, TIE Dar es salaam

SHERIA ZA SHULE

Katika jamii ni lazima kuwepo na sheria na kanuni ili kila mmoja aishi katika hali ya amani, usalama na utulivu. Aidha kuona kuwa kila mmoja anatendewa haki. Shule ya Sekondari Kikaro ni sehemu ya jamii hivyo inastahili kuwa na sheria za kuwaongoza na kuwalinda.

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule kama zilivyoanishwa kwenye mahitaji ya wanafunzi na si vinginevyo.
2. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shuleni na kufuata ratiba iliyowekwa
3. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtulivu na mkimya wakati wote anapokuwa darasani, mistalini na wakati wa kulala. Pia anatakiwa kuwepo darasani wakati wote kama hajaruhusiwa kutoka njee na kiongozi wa darasa au mwalimu.
4. Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au mwanafunzi na mwalimu ni ya lugha ya kiingereza na si vinginevyo
5. Mwanafunzi anatakiwa kukaa shuleni wakati wote wa shule na ni marufuku kuvuka eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu wa zamu. Pia ;
    i. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutoka njee ya MIONO bila ya ruhusa **ya MWALIMU WA MALEZI, MAKAMU MKUU WA SHULE NA MKUU WA SHULE**
    ii. Wageni wote wafike ofisi ya malezi au matron kabla ya kuonana na mwanafunzi husika
    iii. Wanafunzi wa hostel watatembelewa jumapili ya mwisho wa mwezi tu
    iv. Wanafunzi wa hostel wataenda sokoni kila jumatano ya mwisho wa mwezi baada ya masomo.
6. Kila mwanafunzi anatakiwa kuonesha heshima ya hali ya juu kwa ;
    i. Kumsalimia kila mtu anayemzidi umri
    ii. Kumpokea mzigo.
    iii. Kutii bendera taifa kwa kusimama na kukaa mguu sawa inapopandishwa au kushushwa kwa mwongozo wa filimbi au mimbo wa taifa.
    iv. Kutii wimbo wa taifa unapoimbwa
    v. Kuwaheshimu viongozi wa serikali ya wanafunzi
    vi. Ni kosa kutoa kauli chafu au matusi, kupigana na kukashifiana na mwanafunzi mwenzio au mwalimu.
7. Kila mwanafunzi lazima awe nadhifu wakati wote ndani ya eneo la shule na nje ya shule. Ni marufuku kuvaa sketi fupi, nguo za kubana mwili, na ni kosa kuvaa kofia eneo la shule.

8. Ni jukumu la kila mwanafunzi kuhakikisha kuwa anatimiza wajibu wake kwa kushiriki kikamilifu katika kazi zote za elimu ya kujitegemea na utunzaji wa mzingira. Ni kosa kuharibu mazingira kwa kutupa karatasi ovyo, kuchoma moto na kukatiza kwenye viunga.

9. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa mwaminifu na mtunzaji wa mali za umma, pia ni kosa kusema uongo, kuiba na kuficha maovu.
10. Hairuhusiwi msichana kuingiza mvulana au mvulana kuingiza msichana bwenini.

KUMBUKA

Makosa yafuatayo yatamfanya mwanafunzi kufukuzwa shule.

i. Wizi

ii. Kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi (Uasherati/ushoga)

iii. iii. Kuvuta bangi, sigara na kutumia madawa ya kulevya.

iv. iv. Kuharibu makusudi mali ya umma.

v. Kupata kesi ya jinai kufuatana na sheria za nchi.

vi. Kupigana na kumnyanyasa mwanafunzi, mwalimu au mtu yeyote.

vii. Kudharau bendera ya taifa na kukosa utii kwa masuala ya kitaifa.

viii. Kuoa au kuolewa.

ix. Kupata au kusababisha mimba.

x. Kutohudhuria masomo kwa muda siku tisini (90) mfululizo.

xi. Kugoma na kuhamasisha mgomo.

xii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu,/ walezi na jamii kwa ujumla.

xiii. Kushiliki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi;

xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

…….

EMMANUEL J KAHABI

MKUU WA SHULE